JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2023

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2023

# 01 KISWAHILI

*Kimechapishwa na;*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI.....iv

1.0 UTANGULIZI..... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI..... 2

2.1 Sehemu A: Imla..... 2

2.2 Sehemu B: Nyakati Mbalimbali..... 8

2.3 Sehemu C: Kutegua Vitendawili..... 13

2.4 Sehemu D: Utungaji..... 18

2.5 Sehemu E: Ufahamu..... 23

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI 28

4.0 HITIMISHO..... 29

5.0 MAPENDEKEZO..... 30

KIAMBATISHO NA. 1: UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI……….32

KIAMBATISHO NA. 2: ULINGANIFU WA UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI……….33

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2023. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa shule, watunga mitaala, na wadau wengine wa elimu kuhusu sababu zilizochangia ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili. Vilevile, taarifa hii inaonesha jinsi ufundishaji na ujifunzaji ulivyomwezesha au kushindwa kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka minne.

Aidha, taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa usahihi. Baadhi ya sababu hizo ni kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu swali husika, na athari ya lugha mama. Mtawanyiko wa majibu ya wanafunzi kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi kwa kutumia vielelezo, chati na maelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa taarifa hii itawawezesha walimu na wasimamizi wa elimu kubuni mbinu zitakazosaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Kadhalika, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi, yatasaidia kuongeza umahiri wa wanafunzi na hatimaye kuimarisha ubora wa elimu nchini.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inatoa mrejesho wa namna ambavyo wanafunzi walijibu maswali katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2023. Upimaji huu ulizingatia matakwa ya muhtasari wa mwaka 2015 unaolenga kuimarisha umahiri wa mwanafunzi katika Stadi za Kuzungumza, Kusikiliza, Kusoma na Kuandika.

Upimaji wa somo la Kiswahili ulikuwa na sehemu tano. Sehemu A ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusikiliza matamshi ya silabi, maneno, sentensi na kuyaandika (imla). Sehemu B ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kufahamu nyakati mbalimbali kupitia sentensi alizopewa. Sehemu C ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kukamilisha vitendawili kwa kuchagua maneno yaliyopo kwenye mabano na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi. Sehemu D ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kupanga sentensi zilizochanganywa ili ziwe katika mtiririko unaoleta maana kwa kuandika herufi A, B, C, D na E. Sehemu E ililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma na kuelewa maudhui yaliyomo katika shairi. Sehemu hizo zilitoka katika umahiri mkuu wa *kuwasiliana katika miktadha mbalimbali* na *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*. Kila sehemu ilikuwa na swali moja (1) lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama kumi (10).

Jumla ya wanafunzi 1,693,438 walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2023. Kati yao, wanafunzi 1,544,856 walifanya upimaji katika somo la Kiswahili ambapo wanafunzi 1,299,728 sawa na asilimia 84.15 walifaulu.

Viwango vya ufaulu kwa kuzingatia majibu ya wanafunzi vimegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu hizo zimewekwa katika makundi mawili kulingana na alama walizopata. Kundi la kwanza linahusisha swali la 1 na 5, kiwango hafifu ni kati ya alama 0 - 2.5, kiwango cha wastani ni 3.0 - 6.0,

kiwango kizuri 6.5 - 9.5 na kiwango kizuri sana ni alama 10.0. Aidha, kundi la pili linahusisha swali la 2, 3 na 4, kiwango hafifu ni kati ya alama 0 – 2.0, kiwango cha wastani ni 4.0 - 6.0, kiwango kizuri ni alama 8.0 na kiwango kizuri sana ni alama 10.0. Wanafunzi waliokuwa na kiwango cha wastani hadi kiwango kizuri sana ndio waliohesabika kuwa wameweza kujibu maswali kwa usahihi. Aidha, waliopata kiwango hafifu walihesabika kuwa wameshindwa kujibu maswali kwa usahihi.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa wanafunzi katika kila swali umewasilishwa kwa njia ya chati. Rangi mbalimbali zimetumika kubainisha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi kwa kila swali ambapo rangi nyekundu imetumika kuwakilisha kiwango hafifu cha ufaulu, yaani asilimia 0 – 33, rangi ya njano kiwango cha wastani yaani asilimia 34 – 66 na rangi ya kijani imetumika kuwakilisha kiwango kizuri na kizuri sana yaani asilimia 67 - 100.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Sehemu hii inachambua majibu ya wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwa kila sehemu. Aidha, idadi na asilimia ya wanafunzi waliojibu vizuri au walioshindwa kujibu kwa usahihi imeoneshwa katika chati. Vilevile, taarifa hii imeonesha sababu za ufaulu wa wanafunzi kwa kila swali. Sampuli za majibu ya baadhi ya wanafunzi zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu hafifu, wastani na mzuri katika maswali.

### 2.1 Sehemu A: Imla

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la imla ambalo lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali*. Wanafunzi walitakiwa kusikiliza kwa makini sentensi tano (05) walizosomewa kwa sauti kisha kuziandika kwa usahihi. Kila sentensi ilikuwa na maneno manne yenye

alama nusu ($00^1/_2$) kwa kila neno. Kila sentensi ilikuwa na alama 2; hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 10.

Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kusikiliza na kuandika sentensi kwa kuzingatia kanuni za uandishi kama vile; kuanza na herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi, kuweka alama ya nukta mwishoni mwa sentensi pamoja na kutambua sauti mbalimbali za matamshi ya silabi, maneno, na sentensi. Swali hilo linaoneshwa kama ifuatavyo:

**Swali la 1**: **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) ______________________________________________

(ii) ______________________________________________

(iii) ______________________________________________


(iv) ______________________________________________

(v) ______________________________________________

Zifuatazo ni sentensi walizosomewa wanafunzi:

(i) Nywele zako ni fupi.
(ii) Gharama ya umeme imezidi.
(iii) Mheshimiwa Rais amehutubia bunge.
(iv) Amesimama ng'ambo ya mto.
(v) Ndoo hii ni chafu.


Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,544,856 (100%) waliofanya upimaji. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri kwani wanafunzi 1,324,438 (85.73%) walifaulu. **Chati Na. 1** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi hao kwa asilimia.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 186,642 (12.08%) walifanya vizuri sana kwani waliweza kuandika maneno yote ishirini kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika stadi ya kusikiliza na kuandika kwani waliweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano walizosomewa. Pia, waliweza kubaini sauti zinazounda maneno yaliyosomwa na kuziandika kwa usahihi huku wakizingatia kanuni za uandishi, herufi sahihi (fonimu) za maneno husika, matumizi ya herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi na kuweka alama ya kituo mwishoni mwa sentensi.

Vilevile, wanafunzi hao walikuwa na ujuzi wa kubaini na kuandika silabi zenye herufi mwambatano kama vile, silabi ‘*‘nywe’’*, *“gha”*, “*shi*”, ‘‘*nge’’*, ‘‘*ng’a,* ‘‘*mbo’’,* na ‘‘*ndo’’,* kwenye maneno kama vile, “*nywele*”, “gharama”, “*mheshimiwa*”, “*bunge*”, “ng’ambo”, na “*ndoo*” mtawalia. Maneno hayo ni miongoni mwa maneno yaliyounda sentensi tano za imla walizosomewa. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano kwa kuzingatia kanuni za uandishi na hivyo kupata alama zote 10.



1. **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Nywele zako ni fupi

(ii) Gharama ya umeme imezidi.

(iii) Mheshimiwa Rais amehutubia bunge.


(iv) Amesimama ng'ambo ya mto.

(v) Ndoo hii ni chafu.

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1

Hata hivyo, wanafunzi 904,630 (58.56%) walifanya vizuri kwa kupata kuanzia alama 6.5 hadi 9.5 kutokana na kushindwa kuandika kwa usahihi baadhi ya maneno. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusikiliza na kuandika kwa kuzingatia matamshi ya herufi zinazounda maneno kwa kuzingatia kanuni za uandishi lakini walishindwa kuandika kwa usahihi maneno yote.

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 233,166 (15.09%) walipata alama za wastani. Wanafunzi hao waliweza kuandika maneno 6 hadi 12 kati ya maneno 20 ya sentensi zote tano. Aidha, walishindwa kuandika baadhi ya maneno yenye silabi za herufi mwambatano. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi badala ya kuandika neno “Ng’ambo” waliandika “*ngambo*”, “gharama” waliandika “*galama*”. Wengine walishindwa kuzingatia alama za uandishi kwani walianza sentensi kwa herufi ndogo badala ya herufi kubwa na hawakuweka nukta mwishoni mwa sentensi. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi baadhi ya maneno na kushindwa mengine hivyo, kupata alama za wastani.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Nywele Zako nifupi .

(ii) Galama yaumeme Imezidi .

(iii) Mweshimia raisi amekutubiwa bunga .

(iv) Amesimama ng'ambo ya mto .


(v) Ndo hi ni chafu .

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 1

Kielelezo Na.1.2 kinaonesha kuwa mwanafunzi aliweza kuandika kwa usahihi maneno 11 kati ya 20. Maneno aliyoshindwa kuandika ni Gharama aliandika *Galama*, imezidi aliandika *Imezidi* (alianza na herufi kubwa mwanzoni mwa naeno husika) Rais, aliandika *raisi* (Hakuanza na herufi kubwa katika jina husika) amehutubia aliandika *amekutubiwa*, bunge aliandika *bunga*, Ndoo aliandika *ndo*, hii aliandika *hi*, Aidha, mwanafunzi huyo alishindwa kutenganisha maneno kama vile; ni fupi aliandika *nifupi*, ya umeme aliandika *yaumeme* hivyo, kusababisha kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi 220,418 (14.27) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa sababu walishindwa kuandika kwa usahihi maneno waliyosomewa. Baadhi yao hawakuacha nafasi kati ya neno moja na neno lingine huku wengine wakitenganisha silabi za neno moja na silabi nyingine katika kuunda neno. Wengine waliandika maneno bila kuzingatia kanuni za uandishi ambapo walichanganya herufi kubwa na ndogo. Pia, wapo wanafunzi walioanza na herufi ndogo mwanzoni mwa sentensi na kutokuweka alama ya kituo mwishoni mwa sentensi. Kielelezo Na. 1.3 (a)

na (b) kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kuandika kwa usahihi maneno yote waliyosomewa.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) naNaonNe mamiauki mgn

(ii) kahua


(iii) waZi.

(iv) Sentensi

(v) imetumika

Kielelezo Na. 1.3 (a): Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1

Kielelezo Na. 1.3 (a) kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye alinakili baadhi ya maelekezo yaliyopo kwenye maswali ya karatasi ya upimaji na kujaza sehemu iliyoachwa wazi badala ya kuandika sentensi za imla alizosomewa.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Kana bakaku humanaaba

(ii) kamaNanaba NananKaka

(iii) MinataPaNa ManaKaNata

(iv) BanakakanabaKatak to

(v) Moini taaahaKama te

Kielelezo Na. 1.3 (b): Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1

Kielelezo Na. 1.3 (b), kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye aliandika maneno yasiyoeleweka kutokana na kutokumudu stadi za Kusoma na Kuandika.

## 2.2 Sehemu B: Nyakati Mbalimbali

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5). Swali lilitoka katika umahiri mkuu wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali. Kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2), hivyo, kufanya swali kuwa na jumla ya alama kumi (10). Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini nyakati mbalimbali katika sentensi alizopewa. Swali hili lilikuwa kama ifuatavyo:

**Swali la 2** Sentensi zifuatazo zipo katika wakati gani? **Andika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi. Sentensi (i) imetumika kama mfano.

(i) Kaka anaimba nyimbo vizuri.
<u>Wakati uliopo.</u>

(ii) Daktari alimtibu mgonjwa wetu.

______________________________

(iii) Baba yangu ataandika barua.

______________________________

(iv) Wanafunzi wanafanya mtihani wao.

______________________________


(v) Kuku walitaga mayai mengi.

______________________________

(vi) Baba na mama watalima shamba lote.

______________________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,544,856 (100%). Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kubaini nyakati mbalimbali katika sentensi alizopewa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani. **Chati Na. 2** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 897,486 (58.10%) waliweza kubaini nyakati mbalimbali katika sentensi walizopewa. Miongoni mwao, wanafunzi 508,668 (32.93%) walifanya vizuri sana na

kupata alama zote 10. Wanafunzi hao walikuwa na ujuzi mkubwa wa kubaini nyakati mbalimbali katika sentensi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika kwa usahihi wakati uliotumika katika sentensi walizopewa kama ifuatavyo: Kipengele (ii) *wakati uliopita*, (iii) *wakati ujao*, (iv) *wakati uliopo*, (v) *wakati uliopita*, na (vi) *wakati ujao*.

Vilevile, wanafunzi 147,422 (9.54%) walifanya vizuri swali hili lakini hawakuweza kupata alama zote 10 bali walipata alama 8 kwa sababu walijibu kwa usahihi vipengele vinne na kushindwa kipengele kimoja. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikuwa na umahiri kuhusu nyakati mbalimbali Kielelezo Na. 2. kinaonesha mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama 10.

2. **Sentensi zifuatazo zipo katika wakati gani? Andika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi. **Sentensi (i) imetumika kama mfano.**

   **(i) Kaka anaimba nyimbo vizuri.**

   **<u>Wakati uliopo</u>.**

   **(ii) Daktari alimtibu mgonjwa wetu.**

   Uliopita

   **(iii) Baba yangu ataandika barua.**

   Ujao

   **(iv) Wanafunzi wanafanya mtihani wao.**

   Uliopo

   **(v) Kuku walitaga mayai mengi.**

   Uliopita


   **(vi) Baba na mama watalima shamba lote.**

   Ujao

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2

Kielelezo Na. 2.1, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kubaini kwa usahihi nyakati katika sentensi alizopewa.

Aidha, wanafunzi 241,396 (15.63%) waliofanya swali hili walipata alama za wastani. Wanafunzi hao waliweza kubaini nyakati mbalimbali katika baadhi ya sentensi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliweza kubaini nyakati kwa usahihi katika kipengele (ii) *wakati uliopita*, (v) *wakati uliopita*, na (vi) *wakati ujao*, lakini walishindwa katika kipengele cha (iii) na (iv) kwani aliandika wakati usio sahihi katika kipengele cha (iii) *wakati uliopo* badala ya “wakati ujao” na (iv) *wakati wa timilifu* badala ya “wakati uliopo”. Hii inaonesha kuwa mwanafunzi huyu alichanganya hali na wakati kwani hakuna wakati wa timilifu ila kuna hali timilifu. Wanafunzi wengine waliweza kubaini nyakati katika sentensi (iv), (v) na (vi) kwa kuandika wakati uliopo, uliopita na ujao mtawalia na kushindwa kipengele (ii) na (iii) kwa kuandika wakati ujao na uliopo mtawalia. Kielelezo Na**.** 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi wakati uliotumika katika sentensi tatu na kushindwa sentensi mbili na kupata alama za wastani.


2. Sentensi zifuatazo zipo katika wakati gani? **Andika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi. Sentensi (i) imetumika kama mfano.

(i) Kaka anaimba nyimbo vizuri.

Wakati uliopo.

(ii) Daktari alimtibu mgonjwa wetu.

Wakati uliopita.

(iii) Baba yangu ataandika barua.

Wakati Uliopo.

(iv) Wanafunzi wanafanya mtihani wao.

Wakati timilifu.

(v) Kuku walitaga mayai mengi.

Wakati Uliopita.

(vi) Baba na mama watalima shamba lote.

wakati Ujao.

Kielelezo Na. 2. 2: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani

Kielelezo Na. 2.2, kinaonesha mwanafunzi aliweza kubaini nyakati katika sentensi ya (ii), (v) na (vi), na kushindwa kubaini nyakati katika sentensi ya (iii) wakati ulipo badala ya wakati ujao na (iv) wakati timilifu badala ya wakati uliopo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 647,370 (41.90%) walishindwa kubaini nyakati katika sentensi zote tano na kupata alama 0. Baadhi ya wanafunzi waliandika sentensi katika hali ya ukanushi wengine walirudia kuandika sentensi walizopewa kinyume cha matakwa ya swali. Aidha, wanafunzi wengine walibainisha aina za maneno yaliyopo kwenye sentensi husika na wengine walitoa majibu kwa kuonesha wakati ambao siyo sahihi kwa mujibu wa sentensi husika. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja katika majibu yake aliandika kama vile: Kipengele cha (ii) wakati “ujao” badala ya wakati “uliopita”, (iii) wakati “uliopita” badala ya “ujao”, (iv) wakati “uliyopita” badala ya “uliopo” (v) wakati “uliopo”, badala ya “uliopita” na (vi) wakati “uliopita” badala ya “ujao”. Hata hivyo, wapo wanafunzi wachache walioandika wakati sahihi katika kipengele kimoja tu na kushindwa katika vipengele vinne kama vile: mwanafunzi mmoja aliweza kubaini wakati katika kipengele cha (ii) kwa kuandika wakati “uliopita”, na kushindwa kipengele cha (iii) kwa kuandika wakati “uliopita, iv) “uliyopita” badala ya “uliopo”, (v) “*wakati uliopo*”, na (vi) “*uliopo*”. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kubaini nyakati mbalimbali zinavyojitokeza katika sentensi. Kielelezo Na. 2.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

2. **Sentensi zifuatazo zipo katika wakati gani? Andika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi. Sentensi (i) imetumika kama mfano.**

(i) **Kaka anaimba nyimbo vizuri.**

**Wakati uliopo.**

(ii) **Daktari alimtibu mgonjwa wetu.**

kwa huduma ya kwanza

(iii) **Baba yangu ataandika barua.**

kwa jili yabga

(iv) **Wanafunzi wanafanya mtihani wao.**

kwa umakini

(v) **Kuku walitaga mayai mengi.**

Sana

(vi) **Baba na mama watalima shamba lote.**

kwa jili ya biashara

Kielelezo Na. 2.3: Sampuli ya jibu lisilo sahihi swali la 2

Kielelezo Na. 2.3, kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali. Hivyo, aliongeza maneno yenye lengo la kukamilisha sentensi au maelezo zaidi kuhusu sentensi badala ya kubainisha njeo katika sentensi husika.

## 2.3 Sehemu C: Kutegua Vitendawili

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) na lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza*. Swali lililenga kupima umahiri wa kutegua vitendawili. Jumla ya alama katika swali hili ilikuwa 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 02. Swali hilo ni:

**Swali la 3:** Kamilisha vitendawili vifuatavyo kwa kuchagua maneno yaliyopo kwenye mabano na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Askari wangu mpole lakini adui wanamhara ________ (paka, mbwa, mbuzi)


(ii) Bibi hachoki kunibeba _______(kiti, kochi, kitanda)

(iii) Nyumba yangu ina nguzo moja __________________ (kalamu, uyoga, mlango)

(iv) Mzungu katoka ulaya na mkono kiunoni __________ (mkoba, ndoo, kikombe)


(v) Tajiri wa rangi _____ (nyumba, mawingu, kinyonga)

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,544,856 (100%). Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kutegua vitendawili. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 1,247,843 (80.77%) waliweza kujibu vizuri swali hili. **Chati Na. 3** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 3**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 404,000 (26.15%) walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu. Wanafunzi hao waliweza kuchagua na kuandika majibu sahihi ya kila kitendawili walichopewa katika vipengele vyote vitano. Majibu yao yalionesha kuwa, wana uelewa wa kutosha juu ya kutegua vitendawili. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alichagua majibu sahihi yaliyokamilisha vitendawili husika kama ifuatavyo: (i) *paka* (ii) *kitanda* (iii) *uyoga* (iv) *kikombe* (v) *kinyonga* mtawalia. Vilevile, wanafunzi 396,391 (25.66%) walichagua na kukamilisha kwa usahihi vitendawili vinne na kushindwa kitendawili kimoja; hivyo kupata alama 8. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote vya swali kwa usahihi.



**3. Kamilisha vitendawili vifuatavyo kwa kuchagua maneno yaliyopo kwenye mabano na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi.**

(i) Askari wangu mpole lakini adui wanamhara paka.
(paka, mbwa, mbuzi)

(ii) Bibi hachoki kunibeba Kitanda.
(kiti, kochi, kitanda)

(iii) Nyumba yangu ina nguzo moja uyoga.
(kalamu, uyoga, mlango)

(iv) Mzungu katoka ulaya na mkono kiunoni Kikombe.
(mkoba, ndoo, kikombe)

(v) Tajiri wa rangi Kinyonga.
(nyumba, mawingu, kinyonga)

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 447,452 (28.96%) walipata alama za wastani kuanzia 4 hadi 6 kutokana na kutegua kwa usahihi vitendawili viwili hadi vitatu kati ya vitano. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliweza kutegua vitendawili katika kipengele cha (ii) *Bibi hachoki kunibeba*

kuwa ni "*kitanda*", (iii) *Nyumba yangu ina nguzo moja* kuwa ni "*uyoga*", na kipengele cha (iv) *Mzungu katoka ulaya na mkono kiunoni* kuwa ni "*kikombe*". Hata hivyo, alishindwa kukamilisha kwa usahihi kipengele (i) *Askari wangu mpole lakini adui wanamhara* kuwa ni "*mbwa*" badala ya "paka" na kipengele (v) *Tajiri wa rangi* kuwa ni "*mawingu*" badala ya "kinyonga", Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.

3. Kamilisha vitendawili vifuatavyo kwa kuchagua maneno yaliyopo kwenye mabano na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Askari wangu mpole lakini adui wanamhara Mbwa.
(paka, mbwa, mbuzi)

(ii) Bibi hachoki kunibeba Kiti.
(kiti, kochi, kitanda)

(iii) Nyumba yangu ina nguzo moja UYoga.
(kalamu, uyoga, mlango)

(iv) Mzungu katoka ulaya na mkono kiunoni Mkoba.
(mkoba, ndoo, kikombe)

(v) Tajiri wa rangi Kinyonga.
(nyumba, mawingu, kinyonga)

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 3

Kielelezo Na. 3.2, kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani kwa kuweza kukamilisha kwa sahihi vitendawili husika katika kipengele cha (iii) na (v) na kushindwa kipengele cha (i), (ii) na (iv).

Kwa upande mwingine, wanafunzi 297,013 (19.23%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.0. Baadhi yao waliandika nahau na wengine waliandika methali badala ya kutegua vitendawili walivyopewa. Kama vile, (i) *haba na haba hujaza kibaba* (ii)

*hakuna marefu yasiyokuwa na incha* (iii) *haraka haraka haina haraka* (iv) *baniani mbaya kiatu chake dawa* na (v) *asiyesikia la mkuu huvunjika guu*. Hata hivyo, wapo wanafunzi walioandika vitendawili vingine katika maswali husika na wengine walitoa majibu yasiyo sahihi na kushindwa kukidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika majibu ya vitendawili husika ambayo siyo sahihi katika vipengele vyote vitano kama vile; (i) *ugali*, (ii) *kiazi*, (iii) *yai*, (iv) *Hatuimu langoni*, na kipengele cha (v) *Anara nginyingi*. Maana ambazo hazikuakisi majibu sahihi ya vitendawili husika. Aidha, mwanafunzi mwingine alitoa majibu kama vile, (i) *mbuzi*, (ii) *kiti*, (iii) *kalamu* (iv) *mkoba*, na (v) *mawingu*. Kielelezo Na. 3.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

3. Kamilisha vitendawili vifuatavyo kwa kuchagua maneno yaliyopo kwenye mabano na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Askari wangu mpole lakini adui wanamhara E
(paka, mbwa, mbuzi)

(ii) Bibi hachoki kunibeba C
(kiti, kochi, kitanda)

(iii) Nyumba yangu ina nguzo moja A
(kalamu, uyoga, mlango)

(iv) Mzungu katoka ulaya na mkono kiunoni C
(mkoba, ndoo, kikombe)

(v) Tajiri wa rangi C
(nyumba, mawingu, kinyonga)

Kielelezo Na. 3.3: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3

Kielelezo Na. 3.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye hakuelewa matakwa ya swali hivyo, kuandika herufi badala ya kuchagua neno linalotegua vitendawili.

### 2.4 Sehemu D: Utungaji

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2 na kufanya jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kupanga mawazo katika mtiririko unaoleta mantiki. Swali hilo ni:

**Swali la 4:** Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuandika herufi A, B, C, D, na E katika nafasi ulizopewa. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Hatimaye Kaposo alipelekwa hospitali. **F**

(ii) Nyuki walikasirika, wakamfukuza na kumuuma Kaposo. ____________________


(iii) Siku moja Kaposo alitoroka shule na kwenda msituni. ____________________

(iv) Alirusha jiwe likapiga kwenye mzinga wa nyuki. ____________________

(v) Alikuwa akitumia manati yake kuwinda ndege. ____________________

(vi) Huko msituni Kaposo alikwenda kuwinda ndege. ____________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,544,856 (100%). Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo wanafunzi 735,957 (47.64%) walipata alama 4.0 hadi 10.0. **Chati Na. 4** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 448,268 (29.02%) walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwani walijibu kwa usahihi vipengele vyote vitano na kupata alama 10. Wanafunzi hao, waliweza kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana na kuandika herufi sahihi (ii) E (iii) A (iv) D (v) C na (vi) B kwa kuwa waliweza kubaini mtiririko wa matukio. Aidha, waliweza kubaini ni tukio gani limeanza na lipi limefuata kutokana na muktadha wa sentensi husika. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote 5 vya swali kwa usahihi.

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuandika herufi A, B, C, D na E katika nafasi ulizopewa. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Hatimaye Kaposo alipelekwa hospitali. **F**

(ii) Nyuki walikasirika, wakamfukuza na kumuuma Kaposo. E

(iii) Siku moja Kaposo alitoroka shule na kwenda msituni. A

(iv) Alirusha jiwe likapiga kwenye mzinga wa nyuki. D

(v) Alikuwa akitumia manati yake kuwinda ndege. C

(vi) Huko msituni, Kaposo alikwenda kuwinda ndege. B

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4

Hata hivyo, wanafunzi 16,689 (1.08%) walifanya vizuri kwa kupata alama 8 kutokana na kushindwa kupanga kwa usahihi sentensi moja kati ya sentensi tano walizopewa. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutunga habari kwani waliweza kupanga sentensi walizopewa katika mtiririko sahihi na kushindwa swali moja tu.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 271,000 (17.54%) walipata alama za wastani kuanzia 4 hadi 6. Wanafunzi hao, waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 kwa usahihi kwani walikuwa na maarifa ya wastani katika kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu kwa usahihi kipengele (ii) *E*, (iii) A na (vi) B na kukosa kipengele cha (iv) C na (v) D. Alipanga hivyo kwa sababu, katika kipengele (ii) aligundua kuwa ndio sentensi ya mwisho kwa sababu huelezea tukio ambalo limefuata baada ya mzinga wa nyuki kurushiwa jiwe. Vilevile, katika kipengele cha (iii) alibaini kuwa ndio sentensi ya kwanza kwa sababu ndio sentensi funguzi katika kifungu hicho kwa kuwa na maneno “siku moja”.

Aidha, katika kipengele cha (vi) alibaini kuwa kutokana na msuko na ujenzi wa matukio sentensi hiyo hufuata baada ya (iii) A kwa sababu kuna maneno yenye uhusiano na mwendelezo wa matukio kutoka tukio la kwanza kwenye sentensi (iii) kuja la pili kwenye sentensi ya (vi). Maneno hayo ni kama vile, "huko msituni". Hata hivyo, mwanafunzi alishindwa kupanga kwa usahihi kipengele cha (iv) akaandika C na (v) D. Mwanafunzi alishindwa kuelewa kuwa sentensi ya (iv) ilitakiwa kuwa D kwa sababu ni sentensi inayofuata baada ya sentensi ya (v) kulingana na msuko wa matukio. Pia, katika kipengele cha (iv) mwanafunzi alishindwa kuelewa kuwa sentensi hiyo ilipaswa kuwa D kwa sababu ni sentensi inayofuata baada ya sentensi ya (v). Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuandika herufi A, B, C, D na E katika nafasi ulizopewa. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Hatimaye Kaposo alipelekwa hospitali. **F**

(ii) Nyuki walikasirika, wakamfukuza na kumuuma Kaposo. E

(iii) Siku moja Kaposo alitoroka shule na kwenda msituni. A

(iv) Alirusha jiwe likapiga kwenye mzinga wa nyuki. C

(v) Alikuwa akitumia manati yake kuwinda ndege. D

(vi) Huko msituni, Kaposo alikwenda kuwinda ndege. B

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani swali la 4

Kielelezo 4.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepanga kwa usahihi vipengele vitatu ambavyo ni; kipengele cha (ii), (iii) (vi) na kushindwa vipengele viwili (iv) na (v) ambavyo aliandika C na D badala ya D na C mtawalia hivyo, kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 808,899 (52.36%) walipata kiwango hafifu cha ufaulu, kuanzia alama 0 hadi 2.0 kwani waliweza kujibu kipengele 1 au kushindwa kabisa. Wanafunzi hao, hawakuwa na umahiri wa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana. Walishindwa kupanga sentensi hizo kwa kuzingatia uhusiano wa maneno na msuko wa matukio katika sentensi walizopewa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alikosa vipengele vyote vitano kwani alishindwa kupanga sentensi kwa kuzingatia msuko wa matukio kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho kwa kuhusianisha na maana katika sentensi za vipengele husika. Kipengele (ii) aliandika A, (iii) B, (iv) C, (v) D na (vi) E. Kielelezo Na. 4.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu na kupata alama za kiwango hafifu.

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuandika herufi A, B, C, D na E katika nafasi ulizopewa. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Hatimaye Kaposo alipelekwa hospitali. F

(ii) Nyuki walikasirika, wakamfukuza na kumuuma Kaposo. D

(iii) Siku moja Kaposo alitoroka shule na kwenda msituni. F

(iv) Alirusha jiwe likapiga kwenye mzinga wa nyuki. B

(v) Alikuwa akitumia manati yake kuwinda ndege. A

(vi) Huko msituni, Kaposo alikwenda kuwinda ndege. E

Kielelezo Na. 4.3: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 4

**2.5 Sehemu E: Ufahamu**

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi wa kusoma shairi na kulielewa. Swali hilo ni:

**Swali la 5:** Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

*Uhai wa binadamu*, *wategemea mimea*,
*Mazingira ni muhimu*, *hakika twategemea*,
*Miti yetu ni adhimu*, *mvua twajipatia*,
*Pokea zangu salamu*, *tuhifadhi mazingira*.

*Kukulinda ni muhimu*, *miti yetu asilia*,
*Juhudi kila awamu*, *kuitunza asilia*,
*Miti ni zao muhimu*, ***samani*** *twajipatia*,
*Pokea zangu salamu*, *tuhifadhi mazingira*.

*Tumeishika hatamu*, *azima kuifikia*,
*Shughuli za binadamu*, *hakika zinachangia*,
*Kuuharibu utamu*, *wa miti na hewa pia*,
*Pokea zangu salamu*, *tuhifadhi mazingira*.

**Maswali**

(a) Mwandishi wa shairi anasisitiza tulitunze zao gani?
________________________________________

(b) Taja faida mbili tunazozipata kutokana na kutunza miti.
(i)________________________________________
(ii)________________________________________

(c) Nini kinasababisha uharibifu wa mazingira?

______________________________________________

______________________________________________

(d) Nini maana ya neno “samani”?

______________________________________________


______________________________________________

(e) Katika ubeti wa pili mwandishi anatoa ujumbe gani?

______________________________________________

______________________________________________


Wanafunzi 1,544,856 (100%) walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani wanafunzi 781,054 (50.56%) walifaulu kwa kupata alama 3.0 hadi 10.0. **Chati Na. 5** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




**Chati Na. 5**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 66,774 (4.33%) walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote 5 na kupata alama 10.0. Hivyo, walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma shairi na kuelewa

maudhui yaliyomo. Hata hivyo, pamoja na wanafunzi hao kufanya vizuri sana na kupata alama 10.0, wanafunzi 177,841 (11.51%) walipata alama 8.0. Hii ni kutokana na wanafunzi hao kujibu kwa usahihi vipengele vinne na kushindwa kipengele kimoja. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi na kukidhi matakwa ya swali katika kila kipengele.



**Maswali:**

**(a) Mwandishi wa shairi anasisitiza tulitunze zao gani?**

miti

**(b) Taja faida mbili tunazozipata kutokana na kutunza miti.**

(i) Miti inatuletea mvua

(ii) Miti inatupa hewa safi

**(c) Nini kinasababisha uharibifu wa mazingira?**

Shughuli za binadamu

**(d) Nini maana ya neno "samani"?**

Ni vitu vilivyo tengenezwa kwa kutumia mbao.


**(e) Katika Ubeti wa pili mwandishi anatoa ujumbe gani?**

Tutunze miti yetu.

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 536,439 (34.72%) walipata alama za wastani kuanzia 3.0 hadi 6.0 kwa sababu hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma na kubaini maudhui yaliyomo kwenye shairi. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu kwa usahihi kipengele (a) *miti*, (c)

shughuli za kibinadamu. Hata hivyo, alishindwa kujibu kwa usahihi vipengele (b) *husababisha mmomonyoko*, (d) *vitu vyenye ghalama kubwa* badala ya “Vyombo au vitu vinavyotengenezwa kwa kutumia mbao kama vile dawati, kiti, meza, kabati, na kitanda”. Pia, katika kipengele (e) alishindwa kuandika kwa usahihi ujumbe uliotolewa na mwandishi katika ubeti wa pili kwa kuandika *miti huleta mathara makubwa kwa binadamu*. Hii inadhihirisha kwamba mwanafunzi huyu hakusoma kwa usahihi neno samani badala yake alisoma kama samahani neno lenye maana ya kuomba radhi. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele kwa usahihi na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingine na kupata alama za wastani.


**Maswali:**

**(a) Mwandishi wa shairi anasisitiza tulitunze zao gani?**

Miti

**(b) Taja faida mbili tunazozipata kutokana na kutunza miti.**

(i) Hutupatia hewa

(ii) Hutupatia matunda

**(c) Nini kinasababisha uharibifu wa mazingira?**

kukata miti ovyo

kuchoma misitu

**(d) Nini maana ya neno “samani”?**

kuomba radhi kwa makosa tunayoyafanya.


**(e) Katika Ubeti wa pili mwandishi anatoa ujumbe gani?**

Kukulinda ni muhimu. Miti yetu asilia

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani kwa kuandika majibu sahihi katika kipengele (a), (b) na (c) na kukosa kipengele (d) na (e). Katika kipengele (d) mwanafunzi aliandika maana ya "samani" ni *kuomba radhi kwa makosa tunayoyafanya* badala ya kuwa ni vyombo au vitu vinavyotengenezwa kwa kutumia mbao kama vile dawati, kiti, meza, kabati na kitanda. Kipengele (e) mwanafunzi alinakili maneno yaliyopo katika mstari wa kwanza katika ubeti wa pili badala ya kutoa ujumbe unaopatikana katika ubeti huo.

Aidha, wanafunzi 763,802 (49.44%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Wanafunzi hao, hawakuwa na umahiri wa kusoma shairi na kuelewa maudhui yaliyomo. Baadhi yao walijibu kwa usahihi kipengele kimoja tu kati ya vitano walivyopewa. Pia, katika kundi hili, wapo wanafunzi walioshindwa kabisa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vitano. Wengine walinakili maneno yaliyopo kwenye beti za shairi walilopewa na kujaza kama majibu ya maswali waliyopewa kinyume cha matakwa ya swali na kupata alama 0. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika majibu kama vile, (a) *zao la chakula* (b) (i) *Miti hutupatia mbao* na (ii) *miti husababisha kichaka kwa wadudu kujificha*, (c) *wanyama*, (d) *vitu vyenye gharama kubwa*. Aidha, kipengele (e) aliandika *miti ni uti wa mgongo wa Mtanzania*. Kielelezo Na. 5.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.


**Maswali:**

(a) Mwandishi wa shairi anasisitiza tulitunze zao gani?

pokea zangu sulamu

(b) Taja faida mbili tunazozipata kutokana na kutunza miti.

(i) Mazingira nimuhimu

(ii) walegemea mimea

(c) Nini kinasababisha uharibifu wa mazingira?

wamiti na hewa pia

tuhifazimazingira

(d) Nini maana ya neno "samani"?

Vitabu

madawati

(e) Katika Ubeti wa pili mwandishi anatoa ujumbe gani?

barua

Ankini

Kielelezo Na. 5.3: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5

Kielelezo Na. 5.3, kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyenakili maneno kutoka katika beti za shairi alilosoma katika kipengele (a), (b), na (c). Aidha, katika kipengele (d) na (e) mwanafunzi alitoa majibu ambayo hayana uhusiano na shairi alilosoma.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Upimaji wa somo la Kiswahili umehusisha umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali na Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma*. Upimaji huu ulikuwa na maswali matano ambayo yalipima uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza na kuandika sauti mbalimbali za matamshi ya maneno katika sentensi (Imla), umahiri wa kutumia nyakati

mbalimbali, kutegua vitendawili, utungaji ambapo walipanga mawazo katika mtiririko unaoleta maana pia kusoma na kujibu maswali yatokanayo na shairi.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali* ulipimwa katika swali la 1, 2 na 4 na ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 63.82. Aidha, umahiri wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma* ulipimwa katika swali la 3 na 5. Umahiri huo ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 65.66. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi kwa mwaka 2022 na 2023, kinaonesha kupanda kwa ufaulu katika vipengele vya umahiri vilivyotahiniwa mwaka 2023. Viwango vya ufaulu katika mwaka 2023 vikilinganishwa na mwaka 2022 vinaonesha kuwa, katika umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali,* kiwango cha ufaulu kimepanda kutoka asilimia 51.84 hadi asilimia 63.82; hivyo ufaulu umepanda kwa asilimia 11.98. Pia, katika umahiri wa *kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma*, kiwango cha ufaulu kimepanda kutoka asilimia 55.38 hadi 65.66 sawa na ongezeko la asilimia 10.28. Taarifa za uchambuzi huu zimeambatanishwa kwenye Kiambatisho Na. 1 na 2.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla ufaulu wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Kiswahili 2023 ni mzuri kwa sababu wanafunzi 1,299,728 sawa na asilimia 84.15 walifaulu katika upimaji huo kwa kupata alama 10 hadi 50. Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kusikiliza na kuandika sauti mbalimbali za matamshi ya silabi, maneno na sentensi, kutumia nyakati mbalimbali, kutegua vitendawili, kupanga mawazo katika mtiririko unaoleta maana (utungaji). Pia, kusoma na kujibu maswali yaliyotokana na shairi.

Aidha, jumla ya wanafunzi 244,851 sawa na asilimia 16.75 walikuwa na ufaulu hafifu. Wanafunzi hao walishindwa kujibu maswali kwa ufasaha

kutokana na changamoto mbalimbali kama vile: kutokumudu stadi za Kusoma na Kuandika, athari ya lugha mama, kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa umahiri wa kutegua vitendawili, kukosa umahiri wa kupanga mawazo kwenye mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuonesha nyakati mbalimbali katika sentensi.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Pamoja na ufaulu mzuri katika somo la 01 Kiswahili, hatua za makusudi hazina budi kuchukuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa miaka ijayo. Hatua hizo ni kama zifuatazo*:*

(i) Walimu wawaongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya kutosha ya kutumia maneno yenye silabi mwambatano kama ''*nywe''*, *"gha"*, "*shi"*, ''*nge''*, ''*ng'a,* ''*mbo''* na ''*ndo''* kwenye maneno kama vile "*nywele*", "gharama", "*mheshimiwa*", "*bunge*", "ng'ambo" na "*ndoo*" mtawalia na yanayofanana na hayo. Hii itawawezesha wanafunzi kumudu kutamka na kuandika maneno yanayoundwa na herufi hizo.

(ii) Walimu wawaongoze wanafunzi kufahamu nyakati mbalimbali katika sentensi kwa kutumia kadi za manila, chati na maigizo. Hii itasaidia kuwawezesha wanafunzi kuwa na umahiri wa kujua wakati uliopo, ujao, uliopita na hali timilifu ili kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.

(iii) Walimu wawaongoze wanafunzi kufahamu vitendawili na maana zake kwa kutumia njia ya majadiliano, matini, hadithi na picha. Hii itasaidia ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi na kuwawezesha kuwa mahiri katika kutega na kutegua vitendawili katika kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma.

(iv) Walimu wawaongoze wanafunzi kufahamu utungaji wa habari fupi hususani kupanga mawazo kwenye mtiririko unaoleta mantiki kwa kutumia picha, vitu halisi na njia ya vikundi. Hii itawasaidia wanafunzi kurahisisha mawasiliano katika miktadha mbalimbali.

(v) Walimu wawaongoze wanafunzi katika kusoma mashairi na kuelewa maudhui yaliyomo kwa kutumia njia ya vikundi na matini mbalimbali. Hii itawajengea wanafunzi uwezo wa kufanya uchambuzi makini katika mashairi ili kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma.

**KIAMBATISHO NA.1**

## UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2023

| Na. | Umahiri Mkuu | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) Maoni | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 3 | 80.77 | 65.66 | Wastani |
| | | 5 | 50.56 | | |
| 2. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 85.73 | 63.82 | Wastani |
| | | 2 | 58.10 | | |
| | | 4 | 47.64 | | |

**KIAMBATISHO NA.2**

## ULINGANIFU WA UFAULU WA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2023 NA SFNA 2022

| Na. | Umahiri Mkuu | Upimaji 2023 | | | | Upimaji 2022 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 85.73 | 63.82 | Wastani | 1 | 82.10 | 51.84 | Wastani |
| | | 2 | 58.10 | | | 4 | 35.34 | | |
| | | 4 | 47.64 | | | 3 | 38.08 | | |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 3 | 80.77 | 65.66 | Wastani | 5 | 63.20 | 55.38 | Wastani |
| | | 5 | 50.56 | | | 2 | 47.56 | | |